



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI
ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA

Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri, SLP 113, Iselamagazi, SHINYANGA
Simu/Fax: 0282-986382 Barua pepe: info@shinyangadc.go.tz
Website: www.shinyangadc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. SDC.S1/10/X1/22

04.11.2022

WATENDAJI WA VIJJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA,

TANGAZO LA KAZI

SOMO: AJIRA ZA MUDA ZA USIMAMIZI WA MRADI (PWP)

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga anawatangazia watu wote wenye sifa ya kufanya kazi ya Usimamizi wa Miradi ya Ajira za Muda kwa walengwa wa Mpango wa Kususuru Kaya Maskini (TASAF). Muombaji awe na vigezo vifuatazo;

1. Sifa za Mwombaji.

- **Ajue kusoma na kuandika**
- Awe na uwelewa /ujuzi unaothibitika katika fani za ufundi Sanifu (ujenzi/ukarabati wa malambo, Ujenzi na ukarabati wa barabara, visima vya asili na visima vifupi), uhifadhi/usimamizi wa Mazingira, Ardhi na misitu
- Utayari wa kusimamia viwango vya kazi zitakazofanyika kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi katika miradi ngazi ya jamii;
- Awe na uzoefu wa kazi ya usimamizi wa shughuli za kijamii;
- Mwombaji aonyeshe/eleze kazi za mfano alizowahi kuzifanya.
- Kipaumbele kitatolewa kwa mwenyeji mwenye sifa kutoka katika kijiji husika au kijiji jirani.
- Asiwe kiongozi wa Serikali au Chama chochote.
- Awe na uelewa wa msingi wa matumizi ya teknolojia ya upashanaji habari kwa njia ya kielektroniki (Kishikwambi au Simu janja)

2. Uwajibikaji.

- Msimamizi wa Mradi ngazi ya Kijiji atachaguliwa na serikali ya kijiji kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa na kamati ya usimamizi wa mradi;
- Atakuwa anawajibika na kutoa taarifa kwa kamati ya usimamizi wa mradi.

3. Kazi na Majukumu:

- Kuwapangia walengwa kazi kwa kufuata vipimo vya kazi vilivyoidhinishwa;
- Kuchukua orodha ya mahudhurio ya watu wanaofanyakazi kwa kufuata mfumo ulioidhinishwa;
- Kuhakiki orodha ya vifaa, vitendea kazi na malighafi za ujenzi.
- Kuandaa na kutunza orodha ya kila siku kwa ajili ya walengwa wote walio kazini;
- Kuandaa na kuwasilisha taarifa za Wiki/Mwezi kwa kazi inayoendelea kufanyika kwa kufuata Programu ya utekelezaji iliyopitishwa;
- Kuandaa orodha ya walengwa wote waliofanyakazi na kuiwasilisha kwa Mratibu wa Mpango wa Wilaya kwa ajili ya kufanya maandalizi ya malipo;
- Kushirikiana na wataalam wa kisékta kuhakikisha kazi zinafanyika kwa ufanisi na viwango vilivyowekwa vinafikiwa.

4. Eneo la Kazi;

- Eneo la kazi litakuwa katika Kijiji/Kitongoji mradi unapotekelzwa.
- Kazi hii haitakuwa na mshahara ila Kutakuwa na posho kwa yule atakayechaguliwa.

5. Maombi yatumwe kwa:

Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji ambacho mwombaji ameomba.

Waombaji wenye sifa tuu wataitwa kwenye usaili.

Mwisho wa kutuma maombi haya ni tarehe 12/11/2022



Dr. Nice R. Munissy

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA
SHINYANGA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. #3
SHINYANGA**